**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 02 Machi, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**
Taarifa ya Serikali juu ya Nyongeza ya Makadirio ya Ziada na Marekebisho ya Mafungu mbali mbali Yanayotokana na Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**
Taarifa ya Serikali juu ya Hali ya Utekelezaji wa Programu ya Kuhuisha Uchumi na huduma za Jamii kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha la Dunia (IMF).

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**
Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Taarifa ya Nyongeza ya Makadi`rio ya Ziada na Marekebisho ya Mafungu mbali mbali Yanayotokana na Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**
Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Serikali juu ya Hali ya Utekelezaji wa Programu ya Kuhuisha Uchumi na huduma za Jamii kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha la Dunia (IMF).

## II. MASWALI:

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

102. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Ili Serikali ipate mapato yatokanayo na kodi, ni muhimu sana kutoa uelewa na elimu ya kutosha kwa wadau, wakiwemo wafanyabiashara.

Je, Serikali kupitia Mabaraza ya Biashara, inakaa na wadau wao pamoja na Taasisi za kodi

### Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

76. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa kuwa vifaa tiba vingi vya Kituo cha Afya cha Kojani ni vya muda mrefu na vimeshakuwa chakavu, na kwa kuwa mahitaji ya vifaa hivyo yanaendelea kuhitajika siku hadi siku.

Je, ni lini Wizara itakipatia kituo hicho kipimo cha wingi wa damu “HB machine” pamoja na “Glucoplus machine”.

78. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa kuwa nyumba kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kojani ipo, lakini imeshakuwa chakavu mno na hivyo imekuwa usumbufu mkubwa kwa watumishi wa afya wa kituo hicho.

Je, ni lini Wizara itaifanyia matengenezo nyumba hiyo pamoja na kutoa mazingira mazuri ya chakula kwa watumishi wanaoishi nje ya kisiwa cha Kojani.

82. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Maradhi yasiyoambukiza yamekuwa yakiathiri sana wananchi hata wale wenye umri mdogo. Wataalamu wanaeleza kuwa moja ya sababu ya maradhi hayo ni kubadilisha mtindo wa maisha (life style) na kutofanya mazoezi . Hata hivyo, hivi sasa wananchi wamehamasika kufanya mazoezi.

(a) Katika kuunga mkono juhudi hizo, Serikali haioni haja ya kutoa muda wa saa moja katika muda wa kazi ili watumishi wa umma washiriki mazoezi asubuhi.

(b) Je, Serikali haoni ulazima wa kuongeza kodi baadhi ya vyakula vinavyochangia maradhi yasiyoambukiza ili wananchi wajielekeze kula vyakula vya asili kama walivyofanya wazee wetu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

94. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali:

Muda wa kustaafu watumishi wa umma kwa mujibu wa sheria ni miaka 60 na ni jambo la kawaida kwa waajiri kutunza kumbukumbu zote za watumishi wake.

(a) Kwa nini mara kwa mara walimu hujikuta wakipewa taarifa za kustaafu kwa kuchelewa.

(b) Je, kitendo cha kuwacheleweshea taarifa zao hakiathiri stahiki zao.

(c) Je, ni Wizara gani inayobeba jukumu la kutoa taarifa za kustaafu kwa watumishi wa umma.

146. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali inastahili pongezi kwa jitihada zake za kumjali na kumjengea heshima mwalimu ndani na nje ya mazingira ya kazi. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko ya uwepo wa vitendo vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa Serikali vya kuwavunjia heshima na kuwadhalilisha walimu hasa wakati wa Mbio za Mwenge.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba katika Mbio za Mwenge za mwaka jana (2021) kuna walimu wa Wilaya ya Wete waliolazimishwa kulala na mwenge na kuchezeshwa ngoma bila ridhaa zao.

(b) Je, ni upi wajibu na haki za walimu katika Mbio za Mwenge.

(c) Je, ni gharama zipi za lazima na zipi za hiari zinatakiwa kulipwa na walimu wakati wa Mbio za Mwenge.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

19. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijitahidi sana kuifanya ZFA (sasa ni ZFF) kuwa ni mwachama wa CAF na FIFA. Hata hivyo juhudi hizo zilikwama baada ya uchaguzi wa CAF na kupatikana rais mpya wa shirikisho hilo la soka barani Afrika.

(a) Je, ni hatua gani Serikali inaendelea nayo ukizingatia bado wapenda soka wengi wanatamani Zanzibar kujiunga na mashirikisho hayo.

(b) Kwa kuwa Tanzania inawakilishwa na TFF kwenye mashirikisho hayo Je, Zanzibar inafaidika vipi na uwakilishi huo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

51. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali katika kupunguza changamoto ya usafiri na kuboresha miundombinu imepanga kukopa fedha ili kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zote za Zanzibar zenye urefu unakadiriwa kufikia kilomita 220.

(a) Je, utafiti wa kina umefanyika ili kujua kuwa zilizoainishwa ndio barabara halisi zilizokusudiwa katika mpango huo.

(b) Je, ni sahihi kwamba baada ya kumalizika ujenzi huo hakutakuwa na taarifa na changamoto ya barabara nyengine kwa Zanzibar hasa barabara za ndani.

(c) Kwa upande wa jimbo la Mpendae ni barabara zipi zitanufaika na mpango huo ukizingatia mahitaji ni makubwa na barabara za ndani ni nyingi.

145. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imekuwa ikiwezesha njia mbali mbali za ajira ili wananchi waweze kujiajiri na kujipatia kipato kwa njia tofauti ikiwemo umiliki wa gari binafsi za biashara. Hata hivyo, kumekuwa na kero zinazolalamikiwa katika mchakato wa kupasisha gari binafsi za biashara kwa kuwepo vitengo vingi vinavyokaribisha usumbufu na uonevu ikiwemo malipo katika Wilaya na Manispaa.

(a) Je, Serikali inafahamu na kuridhia biashara ya kulazimisha inayofanywa na Mabaraza ya Miji ya kuuza mashati ya madereva na makondakta.

(b) Je, ni upi utaratibu halali unaokubalika na Serikali wa kupasisha gari binafsi za biashara.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kupunguza usumbufu na vituo vya malipo kwa upasishaji wa gari binafsi za biashara.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

134. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shehia ya Jongwe ni shehia kubwa kwa sasa. Maji wanayopata ni maji ambayo yamekuwa na athari ya chumvi na kila muda ukienda mbele hali ya chumvi inazidi.

(a) Je, Mhe. Waziri unalifahamu tatizo la upatikanaji wa maji chumvi katika shehia ya Jongwe.

(b) Je, Wizara itachukua hatuwa gani ili kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wa shehia hiyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu Nam.10 ya 2009 – Kusomwa kwa mara ya Pili.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Taarifa ya Serikali juu ya Nyongeza ya Makadirio ya Ziada na Marekebisho ya Mafungu mbali mbali Yanayotokana na Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Taarifa ya Serikali juu ya Hali ya Utekelezaji wa Programu ya Kuhuisha Uchumi na huduma za Jamii kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 kutoka Shirika la Fedha la Dunia (IMF).

**Zanzibar,**
**02 Machi, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**